*Dar es Salaam*
*28 Agosti, 2026*

Baruapepe: press@ikulu.go.tz

# TAARIFA KWA UMMA

## RAIS SAMIA AWAASA WANUFAIKA WA *"SAMIA SCHOLARSHIP"* KUJENGA UWEZO WA TANZANIA KATIKA TEKNOLOJIA

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema Tanzania inalenga kujenga kizazi cha wataalamu watakaotumia sayansi na teknolojia kutatua changamoto za maendeleo na kuongeza uwezo wa Taifa kiteknolojia.

Amesema hayo leo, tarehe 28 Agosti, 2026, Ikulu jijini Dar es Salaam, wakati akiwaaga vijana 44 wa Kitanzania wanufaika wa ufadhili wa masomo nje ya nchi kupitia Programu ya ***Samia Scholarship.***

Rais Dkt. Samia amesema programu hiyo inalenga kutambua na kuendeleza vipaji vya vijana katika taaluma za kimkakati, ili kuongeza uwezo wa Taifa katika teknolojia, ubunifu na maeneo mengine muhimu kwa maendeleo.

"***Hatutaki kusalia kuwa watumiaji wa kila teknolojia inayoundwa na wengine. Tunataka mkasome, mje muunde hapa,"*** amesema Rais Dkt. Samia, akisisitiza umuhimu wa kujenga uwezo wa ndani wa nchi teknolojia.

Amesema Tanzania ina vijana wenye uwezo wa kushindana kimataifa na kwamba wajibu wa Serikali ni kupanua fursa zitakazowawezesha kukuza vipaji vyao na kuvitumia kwa manufaa ya Taifa.

Rais Dkt. Samia amewataka wanafunzi hao kutumia elimu watakayopata kutatua changamoto za kiuchumi, kijamii na kiteknolojia, na kuongeza tija katika sekta muhimu za maendeleo nchini.

Amesema maarifa hayo yatakuwa na mchango katika utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 na katika kujenga uwezo wa nchi katika teknolojia, utafiti, ubunifu na uzalishaji.



*Ikulu Mawasiliano / ikulu_mawasiliano / ikulu_Tanzania / ikulu Tanzania / ikulumawasilano / Ikulu Tanzania / Ikulu Tanzania*

Aidha, amewataka kuwa wazalendo, waaminifu na wenye nidhamu, huku wakilinda utu, heshima, staha na maadili ya Kitanzania watakapokuwa nje ya nchi.

Amewasisitiza pia kuzingatia sheria za nchi watakazokwenda, kanuni za vyuo watakavyosoma na kulinda jina na heshima ya Tanzania.

Rais Dkt. Samia amezishukuru Serikali za Ireland, Shirikisho la Urusi na Afrika Kusini kwa ushirikiano wao katika programu hiyo, pamoja na NMB, CRDB, Exim Bank na Vodacom Foundation kwa mchango wao.

Vilevile, amewapongeza walimu na wazazi kwa mchango wao katika kuwaandaa vijana hao kitaaluma, kimaadili na kinidhamu hadi kufikia hatua ya kupata fursa za masomo nje ya nchi.

Kwa upande wake, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Adolf Mkenda, amesema Serikali imeendelea kushirikiana na vyuo mbalimbali vya nje ya nchi kupata masharti nafuu ya masomo kwa wanufaika wa Samia Scholarship.

Amesema ushirikiano huo umewezesha kupatikana kwa punguzo la ada na viwango maalum vya malipo, hatua inayosaidia kupunguza gharama za utekelezaji wa programu hiyo.

Programu hiyo ni sehemu ya uwekezaji wa Serikali katika kujenga wataalamu wa kiwango cha juu wa Sayansi ya Data, Akili Unde na fani shirikishi, ili kuongeza uwezo wa Tanzania katika teknolojia, ubunifu na ushindani wa kimataifa.



Bakari S. Machumu
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu